

TAMKO LA WABIBI TANZANIA

WABIBI NI NGUZO YA TAIFA LETU. Tangu Virusi Vya UKIMWI vilipoingia Tanzania, Wabibi tumekuwa tukiwalea watoto wa watoto wetu; yaani, kizazi cha watoto na vijana walioachwa bila ya wazazi kutokana na janga hili. Sisi tulijua kwamba ni lazima kuwalea yatima hawa kwa ukaribu na kuwaonesha upendo. Virusi Vya UKIMWI bado ni tishio katika nchi yetu, lakini Tanzania imeendelea kuhimili kwa sababu sisi Wabibi tumeweka uhimili mkubwa.

Tanzania imeweka historia. Kwa mara ya kwanza hapa Tanzania, Wabibi zaidi ya 200 kutoka pembe zote za nchi tumekusanyika pamoja mjini Arusha, kujumuika pamoja, kujifunza miongoni mwetu wenyewe na kuunda dira ya hali ya hapo baadaye, ambayo tunatamani kuiona kwa ajili ya familia zetu na jamii zetu. Harakati zetu hizi zinakuwa kwa kasi na hatuko peke yetu – tumeungwa mkono na Wabibi kutoka Uganda na Afrika ya Kusini. Upo mshikamano mkubwa. Tunajua kuwa ni lazima tutumie sauti zetu. Wabibi wa Bara la Afrika, tumeamka na kuhamasika kuhusu suala hili.

Hakuna shaka kwamba tunawapenda wajukuu zetu kwa moyo, na tumekwisha kufanya mambo mengi makubwa. Lakini tumegubikwa na mzungu mkubwa. Bibi mmoja kuwalea wajukuu 4 hadi 6, hadi 10, peke yake, siyo jambo jepesi, ni jambo lenye gharama kubwa na lenye simanzi. Vipato vyetu duni, haviwezi kukidhi mahitaji ya familia zetu. Tunapambana sana kuweza kuwapatia chakula watoto hao na kumudu gharama za shule. Matibabu kwa ajili yao kwetu pia ni shida. Haki kuhusiana na ardhi iliyoko chini yetu mara nyingi inatishiwa na kutufanya tunyanyasike zaidi katika kuwalea watoto hawa. Tunakabili na unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI, na kadiri tunavyo endelea kuzeeka, thamani yetu inashushwa na kushushwa tena. TUNAONGEA SASA KWA SABABU TUNAJUA KWAMBA TUKIENDELEA KUFICHA UKWELI, MATATIZO HAYA HAYATA-KWISHA KAMWE.

Wabibi wamesimama bega kwa bega na yatima, lakini ni nani anayesimama kwa ajili yetu Wabibi? Tunaomba tusiachwe peke yetu katika malezi ya kizazi chetu kijacho.

Asasi za kiraia na vikundi vyetu vya kijamii wametuleta pamoja; na kwa mara kadhaa wamekuwa washirika wetu wakuu. Watoto hawa yatima walioko katika jamii zetu ndiyo viongozi wetu wa kesho. Ni watoto wetu sisi sote, na sote tunatakiwa tuwajibike.

Tunatoa wito kwa Taifa letu tukufu la Tanzania kulinda haki zetu, na kuwatunza Wabibi. Tunatambua uwepo wa sera na programu zenye maono mema kama vile TASAF, Tanzania Social Action Fund, lakini misaada yao haitufikii. Mahususi tunao uhitaji wa haraka katika mambo yafuatayo:

- Malipo ya uzeeni kwa Wazee wote, yaani pensheni
- Njia za usaidizi kwa ajili ya mikopo binafsi ya biashara
- Misaada kwa ajili ya watoto wenye hali tete na misaada ya kumudu gharama za elimu katika masomo ya vyo na elimu ya juu
- Huduma za uhakika, za bure na tiba kwa wazee
- Ulinzi kwa ajili ya ardhi na mali zetu
- Kulindwa dhidi ya ukatili, unyanyasaji na ubaguzi vinavyohusishwa na umri, na hali yeyote ile ya ulemavu
- Uwakilishi wa Wabibi katika ngazi zote za kiserikali ikijumuisha uundaji wa kamati za Wabibi katika ngazi za Mitaa hadi Taifa
- Ukusanyaji wa takwimu za Wabibi katika ngazi za chini kabisa hadi Taifa
- Iwepo siku ya Wabibi kitaifa hapa Tanzania
- Itengwe bajeti maalum kwa ajili ya Wabibi katika ngazi zote za serikali

Tunatoa wito pia kwa jumuiya za Kimataifa wawaheshimu Wabibi na kuisaidia Tanzania katika mambo tunayohitaji ili tuweze kusukuma mbele azma yetu hii. Wabibi, kutoka pembe zote za dunia, ikijumuisha kutoka Canada, Australia, Uingereza na Marekani, wametuunga mkono katika mshikamano huu. Tunaziasa serikali zao na wadau wa maendeleo wajiunge nasi katika kufanikisha harakati hizi.

TANZANIA: Tulinde, Tusikilize, na Tupatie fursa. Hatuombi upendeleo. Tunaongea kwa ajili ya haki zetu za kibinadamu na ustawi wetu. Wabibi ni kioo cha jamii yetu. Pale tunapotunza vyema jamii nzima inaimarika.

BIBI NI NGUZO!

KONGAMANO LA WABIBI, ARUSHA, TANZANIA

TAREHE 26 FEBRUARI HADI TAREHE 1 MACHI 2018

